# Wizara ya Mifugo yatoa vifaranga vya samaki

**Na Suleiman Abeid, Shinyanga**

WIZARA ya Mifugo na Uvuvi imetoa msaada wa vifaranga vya samaki 200,000 na vifaranga vingine 200 vya kuku kwa wakazi wa wilaya ya Meatu mkoani Simiyu watakaokuwa tayari kuanzisha ufugaji huo.

Waziri wa Mifugo na Uvuvi nchini, Luhaga Mpina alitoa ahadi hiyo wiki iliyopita katika moja ya mikutano yake ya hadhara katika Jimbo la Kisesa akiwa katika ziara ya kikazi ya kusikiliza changamoto mbalimbali zinazowakabili wafugaji katika jimbo lake.

Mpina alisema hivi sasa wizara yake inawahamasisha wananchi katika suala zima la ufugaji wa samaki katika maeneo yao na kwamba wizara yake tayari imetenga vifaranga vipatayo 2,000 ambavyo vitakuwa vikitolewa bure kwa wananchi watakaoanzisha ufugaji wa samaki.

"Ndugu zangu, niwaombe anzisheni ufugaji wa samaki katika maeneo yenu, samaki watawaingia kipato kizuri iwapo watafugwa kwa kuzingatia kanuni bora za ufugaji wake, wizara yangu imetenga vifaranga laki mbili kwa ajili ya kuwapatia bure wale ambao watakuwa wa kwanza kuanzisha ufugaji huu," alisema.

Alisema wizara yake hivi sasa inahimiza suala la wananchi kuanzisha shughuli za ufugaji wa kisasa iwe kwa wanaofuga ng'ombe, samaki na kuku na kwamba ili ufugaji huo uwe na tija wizara imetenga fungu la fedha kwa ajili ya kutoa mafunzo ya baadhi ya vijana wa Meatu ili wakirejea waweze kuisaidia jamii.

Pia Waziri Mpina alitoa wito kwa wakazi wa Meatu kuanzisha ushirika wa ufugaji wa kuku ambapo alisema kupitia ushirika huyo wizara itakuwa tayari kuwasaidia vifaranga vya kuku wa kisasa na wenye ubora ili waweze kuendesha shughuli za ufugaji.

"Niwapongeze wenzetu wa kata ya Lubiga nasikia tayari wameanzisha vikundi vitatu vya wafugaji kuku, hawa wameonesha mfano, na mimi nawaahidi kuwapatia vifaranga vya kisasa katika hivyo 200 tulivyotenga ili waweze kufuga kuku wenye ubora, lakini pia kupitia ushirika wao watakuwa na fursa ya kupata mkopo kuendelea ufugaji wao," alisema.

Katika hatua nyingine, Mpina alitoa pampu za maji kwa kila kata ambacho kitakuwa kimechimba kisima cha maji na kwamba pampu hizo zipo tayari kinachohitajika ni wanakijiji kuchimba kisima na kisha watapatiwa pampu ya kufunga kwenye kisima hicho.

" Ndugu zangu suala la maji safi na salama bado ni changamoto katika maeneo yetu mengi, lakini binafsi nimekuwa nikijitahidi kusaidia kila pale ninapoweza, sasa hivi kuna pampu za maji zimenunuliwa, kila kata yenye kisima nitawapatia pampu moja," alisema Mpina.

Scanned by CamScanner

Simbaya alisema jamii

ufanisi mkubwa.

kumwongezea uwezo wa kufanya

wao wamekuwa na mabadiliko makubwa na sasa wapo vizuri.



**Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Abdallah Ulega akikagua eneo linalotumika kuchoma nyama kwenye mnada wa Ndelema uliopo katika Halmashauri ya Mji wa Handeni mkoani Tanga wakati akihitimisha ziara yake wilayani humo.** (Na Mpigapicha Wetu)

MAKAMU
Chama Cha
Tanzania Bar
amewahimiza
madhehebu
wasichoke ku
iendelee kuw
kwa kudumis
Mangula al
wakati akizun
mkutano maa
na Wajumbe
Wazee Mani
Alisema an
nchini umesa
na nchi kwa
maendeleo k
kwa kasi.
"Maendele
tunayoyaona
ya barabara
hospitali na
bila amani n
haya ya kujiv
kwa ujumla
kiasi kikubw
maombi ya v
dini," alisema
Mangula a
Uganda ilipo
enzi za Rais
alikuwa mku
Kagera.
Aliwataka
kumi, kuanzi
za watu wat
mwenyewe)
"Majukum
pamoja na k
na utulivu u
kuhimiza uli
uanachama

# CCM yashtushwa na kasi ya ongezeko la samaki

**Na Mwandishi Wetu, Simiyu**

CHAMA cha Mapinduzi (CCM) kimeshtushwa na ongezeko kubwa la samaki aina ya Sangara ikiwa ni miaka mitatu tu tangu Serikali ya awamu ya tano kuanza operesheni za kudhibiti uvuvi haramu katika Ziwa Victoria na kutaka Serikali kuchukua hatua za haraka kutafuta masoko ya uhakika ya samaki ndani na nje ya nchi.

Wakizungumza kwenye ziara ya Wajumbe wa Sektetarieti ya Chama cha Mapinduzi Mkoa wa Simiyu baadhi ya Wavuvi katika Mwalo wa Nyamikoma wilayani Busega wamesema awali kabla ya operesheni kuanza walikuwa wakisafirisha wastani wa tani 6 za samaki kwa mwezi lakini tangu Serikali ilipoamua kuchukua hatua za kudhibiti uvuvi haramu samaki wameongezeka na sasa wanasafirisha wastani wa tani 60 kwa mwezi.

Mwenyekiti wa Kikundi cha Usimamizi wa Rasilimali za Uvuvi ëBMUí Mwalo wa Nyamikoma wilayani Busega mkoani Simiyu , George James alisema ongezeko hilo kubwa la samaki pia limepunguza bei ya Sangara kutoka wastani wa sh. 9,000 kwa kilo hadi kufikia sh. 4,000.

Mbali na mafanikio hayo pia wavuvi hao wameiomba Serikali kuwasaidia kupata mtambo wa kutengeneza barafu katika eneo hilo kwani kwa sasa wanalazimika kusafiri hadi jijini Mwanza umbali wa zaidi ya kilomita 150 kufuata barafu.

Hivyo walimuomba Katibu wa CCM Mkoa wa Simiyu kumfikishia shukrani Rais wa Tanzania, Dkt. John Magufuli, kwa uongozi wake imara hasa katika usimamizi wake wa rasilimali za uvuvi na kwamba sasa samaki ni wengi na kwamba ombi lao kubwa ni kusaidiwa kupata soko baada ya ongezeko hilo la samaki.

Akizungumza katika mkutano wa hadhara uliofanyika katika Mwalo wa Nyamikoma wilayani Busega, Katibu wa CCM Mkoa wa Simiyu, Haula Kachwamba, aliitaka Serikali kupitia Dawati la Sekta Binafsi lililoko Wizara ya Mifugo na Uvuvi kufika katika mwalo huo wa Nyamikoma ili kuwaunganisha wavuvi hao na taasisi za kifedha kuweza kupata mtambo wa kutengeneza barafu.

Pia aliitaka Serikali kutanua wigo wa kuwatafutia masoko ya samaki wavuvi hao ili kunufaika na fursa kubwa ya ongezeko hilo la samaki aina ya Sangara kwa kupeleka katika masoko ya mikoa ya mbali na Ziwa Victoria pamoja na nchi za jirani za Kongo, Zambia, Burundi, Rwanda, Malawi na Msumbiji.

Kuhusu vita dhidi ya uvuvi haramu, Katibu huyo alisema Ilani ya CCM imeitaka Serikali kudhibiti uvuvi ili kupata uvuvi endelevu na kuongeza kipato cha mwanchi mmoja mmoja na kuiletea fedha za kigeni Serikali kutokana na mauzo ya samaki nje ya nchi na kupongeza juhudi kubwa zilizofanywa na Rais Dkt. John Magufuli katika kusimamia rasilimali hizo za uvuvi.

"Tunaishukuru Serikali kwa kuamua na kusimamia operesheni Sangara ambayo ilisimamiwa na Wizara ya Mifugo na Uvuvi operesheni hii imezaa matunda kama mlivyotoa ushuhuda kwamba operesheni hii mliipinga sana lakini sasa mnaona matokeo yake," alisema.

Aliongeza kuwa CCM inaamini katika kusimamia sheria na kwamba hatua zote zilizochukuliwa na Serikali katika kudhibiti uvuvi haramu zililenga kunufaisha Watanzania wengi tofauti na hapo awali ambapo watu wachache ndio waliokuwa wakinufaika kupitia uvuvi haramu.

"Niipongeze sana Serikali yetu kwa kukubali kutukanwa, kuzuliwa maneno mengi kupata kashfa nyingi lakini bado waliendelea kusimamia msimamo wa kulinusuru ziwa letu kwenye ilani yetu tumesema tutahakikisha tunadhibiti uvuvi haramu ili tuweze kupata samaki wa kutosha kwa ajili ya watanzania sisi CCM tunaomba msiishie hapa endeleeni kudhibiti uvuvi haramu ili matunda yazidi kuongezeka siku hadi siku," alisema Katibu wa CCM

Katika hatua nyingine, Mwakilishi wa Mkuu wa Wilaya ya Busega, David Palanjo aliongoza zoezi la uteketekezaji wa shehena ya nyavu haramu zilizokamatwa kwenye operesheni hiyo katika wilaya za Magu na Busega na kutoa wito kwa wananchi kuunga mkono juhudi za Serikali katika kudhibiti uvuvi haramu.

Scanned by CamScanner